# SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 28 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JUNI 2023

# MAGEUZI KATIKA SERA NA MTAALA WA ELIMU YANAZINGATIA MATAKWA YA WANANCHI: PROF. MKENDA




*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza wakati akifungua kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu linalofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# TUIUNGE MKONO SERIKALI KATIKA KUPATA SERA NA MTAALA MPYA WA ELIMU

Serikali imekamilisha rasimu ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 na mapitio ya mitaala mipya ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ambayo inalenga kuleta maboresho makubwa katika elimu yetu ili kusaidia Taifa kupiga hatua zaidi katika maendeleo.

Miongoni mwa mabadiliko yaliyoelezwa katika rasimu hizo ni elimu ya lazima kujumuisha elimu ya msingi na elimu ya sekondari ngazi ya chini ambayo itatolewa kwa miaka 10, masomo ya Kifaransa, Kichina, Kiarabu, Historia ya Tanzania na Maadili na Chakula na Lishe kuongezwa katika madarasa ya elimu ya msingi na sekondari, umri wa kuanza darasa la kwanza umepunguzwa kutoka miaka saba hadi sita.

Mabadiliko mengine ni elimu ya sekondari ngazi ya chini kugawanyika katika mikondo miwili ambayo ni mkondo wa elimu ya jumla na mkondo wa elimu ya amali. Elimu ya sekondari ngazi ya juu au elimu ya amali sanifu itakuwa hitaji la msingi kwa ajili ya kujiunga na elimu ya juu. Pia elimu ya juu itakuwa elimu baada ya elimu ya sekondari na itagawanyika katika mkondo wa elimu ya jumla na elimu ya amali.

Hatuwezi kuainisha mabadiliko yote yanayoelezwa katika rasimu hizo, lakini ni wazi kuwa mabadiliko yote yanayokuja ni yanaisaidia nchi yetu kupiga hatua katika maendeleo. Hivyo, ni muhimu kwa kila mdau wa elimu kuunga mkono jitihada hizi za Serikali ili Sera na Mtaala mpya wa Elimu viweze kupatikana na kuwawezesha vijana wetu kuwa na ujuzi na kujiamini ili kujiajiri na kuajirika kwa maslahi ya Taifa letu.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina M. Nkwama

**Wajumbe**
Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard J. Chami

**Mhariri**
Adili J. Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas G. Ogunde

# KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania   tumeyautumishiwawalimutanzania

# MAGEUZI KATIKA SERA NA MTAALA WA ELIMU YANAZINGATIA MATAKWA YA WANANCHI: PROF. MKENDA

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema Serikali ya awamu ya sita imedhamiria kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu yanayozingatia matakwa ya wananchi, mahitaji ya kijamii na kiuchumi ya sasa na baadae katika mazingira ya utandawazi

Waziri Mkenda aliyasema hayo wakati akifungua kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu linalofanyika kuanzia Mei 12-14, 2023 jijini Dodoma.

Alisema kuwa mageuzi hayo yanalenga kuwezesha wahitimu kuwa na ujuzi na kujiamini ili kujiajiri na kuajirika, hivyo aliwataka washiriki wa kongamano hilo kutoa maoni yao kwa uhuru na uwazi ili kusaidia kuandaa sera na mitaala bora ya elimu.

"Ni matumaini yangu kuwa mtatoa maoni na ushauri ambao utakuwa chachu ya maboresho ya rasimu hii ya Sera na Mtaala wa elimu" alisema.

Hata hivyo alisema kuwa Serikali imedhamiria kufufua na kurudisha shule za sekondari za ufundi ambazo zitaanza kuchukua wanafunzi kuanzia Januari mwakani.

Prof. Mkenda alisema kuwa mapendekezo ya kufufua shule za sekondari za ufundi ni kutokana na vijana wengi kuona kama kusoma ufundi bila kuwa na elimu ya sekondari ni kujidhalilisha.

"Tumetenga bajeti ya kurudisha shule zetu za sekondari ambazo pia zinafundisha masomo ya ufundi, hii ni kwa sababu tumeona vijana wengi wakienda kusoma katika vyuo vya ufundi,wanarudi tena kufanya mtihadi wa kidato cha sita ili waende vyuo vikuu,wakidhani kusoma ufundi ni kujidhalilisha."alisema Prof. Mkenda

Aidha, Waziri huyo amewatoa



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza wakati akifungua kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu lililofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*

hofu walimu waliopo kazini kuwa utaratibu mpya utakapoanza kutumika hautaathiri ajira zao badala yake Serikali itaangalia namna ya kuwapa nafasi ya kwenda kujiendeleza kielimu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo, alisema mapitio ya mitaala kwa vyuo vya ufundi na elimu ya juu nayo yameanza vizuri kwa lengo la kuoanisha na elimu inayotolewa katika ngazi za elimu zinazoanza.

"Katika utekelezaji wa rasimu hiyo kulikuwa na kamati mbili ambazo zimefanya kazi ya kukusanya maoni ambapo zaidi ya wadau 200,000 walifikiwa na kupata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu maboresho ya sera na mitaala ya elimu hapa nchini,"alisema Prof.Nombo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo Prof. Kitila Mkumbo, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kufanya mageuzi hayo ya elimu nchini kwa kuwa kilikuwa kilio cha muda mrefu cha kupitia mfumo wa elimu.

"Kongamano hilo ni fursa kwa wabunge kuchukua maoni na kuyafanyia kazi ili kuhakikisha serikali inayachukua lakini pia kwa yale ya kisheria, Kamati hiyo itahakikisha Sheria inatungwa" alisema Prof. Mkumbo.

Aidha, Prof. Mkumbo alimpongeza Waziri Mkenda na timu yake ya wizara kwa kuwa wepesi kufanyia kazi maelekezo ya Rais ya kupitia sera na mitaala, duniani kote elimu ina mambo matatu, fursa, ubora wa elimu na elimu itolewayo kuwasaidia wanaoipata kujitegemea.

## MAGEUZI KATIKA SERA NA MTAALA WA ELIMU YANAZINGATIA MATAKWA YA WANANCHI: PROF. MKENDA




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, akizungumza wakati wa kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, Msingi, Sekondari na ualimu lililofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, akizungumza wakati wa kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, Msingi, Sekondari na ualimu lililofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*




*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Prof. Kitila Mkumbo, akizungumza wakati wa kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu lililofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*




*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Bi. Rosemary Senyamule, akitoa salamu za mkoa wake wakati wa kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu lililofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*





*Sehemu ya washiriki wakifatilia hotuba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (hayupo pichani), wakati akifungua kongamano la kujadili sera na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu lililofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*

# MKUTANO WA TUME



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati) akiongoza kikao cha Tume kilichofanyika tarehe 02 - 06 Mei, 2023 katika Ukumbi wa Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Pichani, kushoto ni Makamu mwenyekiti wa TSC, Bahati Mgongolwa na Kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*





*Kikao cha Tume kilichofanyika tarehe 02 - 06 Mei, 2023 katika Ukumbi wa Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kikiwa kinaendea.*



# WALIMU WATOA MAONI YAO KONGAMANO LA SERA NA MITAALA YA ELIMU

- *Wapendekeza elimu ya lazima iwe miaka 11*
- *Wataka lugha ya kufundishia iwe kiingereza kuanzia elimu ya awali hadi chuo kikuu*
- *Wataka Lugha ya Kireno na Kihispania ziongezwe*
- *Wataka fani zote katika mkondo wa elimu ya amali zifundishwe katika shule zote*

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Walimu wa shule za sekondari, wakufunzi na wahadhiri wa vyuo mbalimbali, wameshauri elimu ya lazima iwe ya miaka 11 badala ya miaka 10 kama ilivyopendekezwa kwenye rasimu ya sera na mitaala ya elimu.

Aidha, walimu hao wameshauri kuwa falsafa ya elimu iendelee kuwa elimu ya kujitegemea kwani wanadhani bado inatosha kuendelea kuwa falsafa ya elimu ya Tanzania na pia lugha ya kufundishia iwe kiingereza kuanzia elimu ya awali mpaka chuo kikuu na pia lugha ya Kihispania na Kireno ziongezwe.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake kwenye kongamano la sera na mitaala ya elimu mjini Dodoma jana, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Muhange Kakonko mkoani Kigoma, Zamoyoni Uzale alisema kwa maoni yao wanaona hayo yakifanyika yataboresha elimu.

"Pia fani zote katika mkondo wa elimu ya amali zifundishwe katika shule zote ili wanafunzi wachague kulingana na mahitaji… tunadhani kufunga baadhi ya shule kufundisha fani fulani itasababisha wanafunzi wengine kukosa fursa ya kuchagua kulingana na mahitaji yao," alisema Uzale ambaye ni mwalimu wa somo la Historia.

Kuhusu elimu kuwa ya miaka 11 badala ya 10 kama mapendekezo yanavyosema, Uzale alisema sera imeuacha mwaka mmoja wa awali hivyo wanapendekeza umuhimu wa elimu ya awali na hivyo sera itaje elimu lazima iwe ya miaka 11.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wa serikali na taasisi, Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Profesa Preksedis Ndomba alisema muundo wa mfumo wa elimu haujazingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu hasa viziwi, ulemavu wa akili na usonji kwani wanahitaji muda zaidi wa kusoma.

"Kamati imesita kidogo baada ya kuona sera inazungumzia elimu ya amali hasa kufundishwa kulingana na maeneo ya kijiografia, inatoa angalizo kwamba tunaweza kuwa na elimu ya kikandakanda ya kimaeneo inaweza kupunguza ule muingiliano ambao tumeurithi toka uhuru, tamko husika 3.3 11 liboreshwe," alisema profesa Ndomba.

Aidha alisema pia tamko la 3.3.29 liboreshwe kwa kuongeza lugha ya alama ili kurahisisha mawasiliano shuleni kwa wanafunzi wenye uziwi, kutoona.

"Umri wa kuanza shule kwa watoto wenye mahitaji maalumu



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akishiriki kongamano la kujadili Sera na Mitaala mipya ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu linalofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*

# WALIMU WATOA MAONI YAO KONGAMANO LA SERA NA MITAALA YA ELIMU

haujawekwa, kwenye sera iainishwe vizuri maana wale wanaweza kuanza wamechelewa miaka saba, minane kutokana na uchelewaji wa utambuzi," alisema profesa Ndomba.

Mwenyekiti wa Kongamano Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolph Mkenda alisema watazingatia maoni yaliyotolewa kwenye kongamano hilo.

Profesa Mkenda alisema kuhusu suala la tehama, kampuni ya simu ya Airtel wamempa mapendekezo ambayo atayafanyia kazi na kuzitaka kampuni nyingine kujitokeza wafanye kazi.

Naibu Waziri ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Deogratius Ndejembi aliwahakikishia wadau wa elimu kuwa wizara hiyo iko tayari kufanya maboresho na kuifanya elimu ya Tanzania kuwa bora.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Carolyne Nombo alisema alikuwa na lengo la kupata maoni kwenye rasimu ya sera na rasimu ya mitaala na maoni mengi yametolewa.

"Kupitia mjadala huu tumeona maeneo mazuri ya kufanyia kazi na michango yenu itakwenda kuchakatwa tena," alisema profesa Nombo.

Mwakilishi wa wadau wa maendeleo kutoka Shirika la Kuwahudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), Deo Kapichi alisema kuwa mapitio hayo yanakwenda sambamba na mipango ya kimataifa ya mapitio ya elimu.

Makamu mwenyekiti wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), Rose Mariki alisema Rais Samia Suluhu Hassan alikuja na wazo zuri la kuangalia mahali pa kuboresha.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mali Zanzibar, Mtumwa Idd Hamad alisema watashirikiana kuhakikisha azma ya serikali inatekelezwa kwa vitendo.









*Sehemu ya washiriki wa kongamano la kujadili Sera na Mitaala mipya ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu linalofanyika jijini Dodoma tarehe 12-14 Mei, 2023.*

# TSC KUWASAIDIA WALIMU KUIELEWA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU SURA 448 NA KANUNI ZAKE

**Na Mwandishi wetu – Mpanda, Katavi**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amesema TSC inaendelea kutengeneza mazingira rafiki kwa walimu katika kuielewa kwa kina Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016 ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mwl. Nkwama ameyasema hayo Mei 31, 2023 mjini Mpanda mkoani Katavi wakati akifungua kikao kazi cha siku tatu kinachohusisha wadau wa elimu wakiwemo Afisa Elimu wa Mkoa wa Katavi, Watumishi wa TSC Wilaya ya Mpanda na Makao Makuu Dodoma, Maafisa Elimu, Wathibiti Ubora wa Shule, Chama cha Walimu (CWT) na Walimu kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.

Washiriki wa kikao kazi hicho kilichoandaliwa kwa ufadhili wa Mradi wa Shule Bora wana jukumu la kupitia na kufanya maboresho ya rasimu ya Ufafanuzi wa Sheria hiyo kwa lengo la kuiweka katika lugha na tafsiri rahisi itakayoweza kueleweka kwa walimu wote nchini.

Katibu alieleza kuwa walimu wanamekuwa wakifanya kazi kwa bidii jambo ambalo limefanya ufaulu wa wanafunzi kuongezeka, hata hivyo aliweka wazi kuwa wapo walimu wengi ambao hawana uelewa wa kutosha juu ya Sheria na Kanuni hizo zinazosimamia utumishi wao.

"Mwalimu akitulia na kila kitu chake kikitulia kazi yake itakuwa kufundisha watoto tu. Walimu wetu wanafanya



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha wadau wa Elimu kilicholenga kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*

# TSC KUWASAIDIA WALIMU KUIELEWA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU SURA 448 NA KANUNI ZAKE

kazi vizuri lakini tumebaini kuwa wanachangamoto nyingi ikiwemo kutokuifahamu vizuri Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ambayo ndiyo inayosimamia utumishi wao. Tunahitaji mwalimu afahamu kila kitu kinachohusu utumishi wake, hivyo kazi hii ikikamilika itakuwa ni mwarobaini wa utatuzi wa changamoto hiyo," alisema.

Alisema Sheria hiyo pamoja na kanuni zake zimeweka wazi masuala yote yanayohusu namna ya kushughulikia masuala ya Nidhamu, Ajira na Maendeleo ya walimu na pia imeweka vyombo mbalimbali vya kushughulikia masuala hayo.

"Walimu wameheshimishwa sana katika utumishi wao, kwa mfano TSC ngazi ya Wilaya inaundwa na Kamati ya Tume yenye Mwenyekiti, Katibu pamoja na wajumbe wanne (4). Wajumbe hao ni Katibu Tawala Wilaya, Afisa Elimu Wilaya na Walimu wawili (2), mmoja kutoka shule za Msingi na mwingine kutoka Sekondari. Hawa ndio wanaoamua masuala ya Nidhamu na Maendeleo ya Walimu," alisema.



*Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016, wakimsikiliza Katibu wa TSC wakati wa ufunguzi wa kikao kazi kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*




*Mkurugenzi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Mwl. Fatuma Muya akitoa neno la kumkaribisha Katibu wa TSC ili afungue kikao kazi cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*

Aliongeza kuwa mwalimu asiporidhika na uamuzi unaofanywa na TSC Wilaya Sheria imempa fursa ya kukata rufaa Tume Makao Makuu ambayo inaundwa na Mwenyekiti, Katibu pamoja na wajumbe nane kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, na endapo hataridhishwa na uamuzi wa TSC Makao Makuu ana haki ya kukata rufaa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Katika eneo la ajira na maendeleo ya walimu napo kuna changamoto za walimu kutofahamu taratibu. Kwa mfano, hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan ametoa kibali cha kupandisha madaraja watumishi wa Umma wakiwemo walimu, lakini tunapokea simu za malalamiko kutoka kwa walimu

# TSC KUWASAIDIA WALIMU KUIELEWA SHERIA YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU SURA 448 NA KANUNI ZAKE

wakidai hawajapandishwa lakini wengi wao bado hawajakidhi vigezo kulingana na miongozo iliyopo. Hivyo, unaweza kuona kuwa bado tuna kazi kubwa ya kuwaelimisha walimu wetu," alisema.

Pamoja na hayo, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada mbalimbali anazofanya katika kuboresha sekta ya elimu ikiwemo kutafuta wadau mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya elimu, kuanzisha mchakato wa kuandaa Sera na Mtaala mpya wa elimu na kueleza kuwa TSC itahakikisha fedha zote zilizoelekezwa katika Tume hiyo zitatumika kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

"Ninaomba kutumia fursa hii kumhakikishia Mhe. Rais wetu kwamba Tume ya Utumishi wa Walimu tunaithamini kazi kubwa anayoifanya. Tunamwahidi kuwa tutahakikisha thamani ya fedha kwa kazi inayofanyika inapatikana na inaonekana ili malengo ya kuboresha elimu nchini yaweze kufikiwa," alisema.

Akitoa neno la utangulizi, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Elimu Mkoa wa Katavi, Mwl. Upendo Rweyemamu alisema TSC imeendelea kupiga hatua katika kusimamia walimu jambo ambalo limesaidia kuleta utulivu na kufanya walimu kuendelea kutoa huduma kwa walimu.

Vilevile, Mwl. Rweyemamu alishukuru Mradi wa Shule Bora kwa kushirikiana na Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu katika Mkoa wa Katavi huku akisema Serikali itatoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha mipango yote inakamalika bila vikwazo.

"Tunawashukuru wadau wetu wa Shule Bora kwa kuiwezesha Tume kushiriki kwa karibu na kuhakikisha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 inafafanuliwa ili iweze kutumika na kueleweka kwa urahisi kwa walimu wetu na wadau wengine. Tunatambua kuwa mmekuwa na miradi mbalimbali ya elimu ndani ya mkoa wetu, jambo hili linaifanya Katavi kuongeza kasi ya maendeleo katika sekta ya elimu," alisema.

Mradi wa Shule Bora unafanya kazi katika mikoa tisa Tanzania Bara ambayo ni Rukwa, Katavi, Kigoma, Tanga, Pwani Mara Simiyu, Singida na Dodoma.




*Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Katavi anayeshughulikia elimu, Mwl. Upendo Rweyemamu akitoa neno wakati wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*




*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mpanda Benson Ng'amilo akitoa neno la ukaribisho wakati wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa kikao kazi cha wadau wa Elimu cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*



*Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016, wakiwa katika mawasilisho ya kazi za vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu hiyo. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*







*Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016, wakiwa katika kazi za vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu hiyo. Kikao kazi hicho kilifanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.*

# SHULE 57 ZAJENGEWA UWEZO WA UFAFANUZI WA KANUNI ZA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU – AS MASAZA

- *Walimu 645 wa Msingi na Sekondari kutoka Kata 8 wafikiwa;*
- *Wanafunzi 5,586 wa Sekondari wafikiwa na elimu ya Shule Salama;*
- *Kero ya viboko visivyozingatia Sheria na Taratibu yatamalaki;*
- *Walimu 59 wathibitishwa kazini na Kamati ya Tume ya Wilaya;*
- *Mashauri 6 ya Walimu yapokelewa robo ya tatu ya 2022/ 23; na*
- *TSC Mbogwe yajivunia mwitikio na mapokeo chanya ya Walimu.*

**Na. Mwandishi Wetu – Mbogwe.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Mbogwe kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe Mkoani Geita hivi karibuni imefanikiwa kutoa elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Walimu 645 wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka Kata nane Wilayani humo ikiwa ni pamoja na kutoa unasihi kwa Wanafunzi wapatao 5,586 wa Shule nane za Sekondari juu ya masuala yanayohusu shule salama na uzingatiaji wa maadili ya Kitanzania ili kupambana na vitendo viovu vya ukatili na unyanyasaji wa kisaikolojia na kijinsia.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilayani Mbogwe, Mwl. Tamasha Masaza, akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa utoaji elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa ufadhili wa Mradi wa BOOST wilayani humo alipotembelewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, katika ziara zake za kila mwezi kupata habari za utendaji kazi wa Ofisi za Wilaya.

“Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri yetu hapa tunayofanya nayo kazi, hivi karibuni tulifanikiwa kutembelea na kutoa elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Walimu 645 wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka Kata nane kati ya Kata 17 tunazozihudumia hapa Wilayani.” Alisema Kaimu Katibu Msaidizi Mwl. Masaza.

Mwl. Masaza alisema lengo kuu la ziara hiyo lilikuwa ni kufafanua kanuni hizo za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu za mwaka 2023 kwani ufafanuzi huo umetokana na



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mbogwe, Mwl. Tamasha Masaza akizungumzia utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya Mbogwe wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) iliyofanyika wilayani hapo hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji ya majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.*

# SHULE 57 ZAJENGEWA UWEZO WA UFAFANUZI WA KANUNI ZA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU – AS MASAZA

ukweli kuwa walimu wanapaswa kukumbushwa juu ya Kanuni na Sheria zinazohusiana na utendaji kazi wao wa kila siku ili kuepukana na makosa yanayoepukika na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa mashauri mbalimbali ya walimu yanayojitokeza kutokana na kutojua au kutozingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma.

Aliongeza kuwa elimu hiyo ya ufafanuzi wa kanuni kwa Walimu pamoja na mambo mengine ulihusisha vipengele muhimu vikiwemo wajibu wa mwalimu kwa mwanafunzi, Taratibu na Miongozo ya kiutumishi katika kujihusisha au kushiriki katika shughuli za kisiasa, makosa ya jinai, makosa ya kimaadili na mengeniyo yakiambatana na adhabu zake.

Kaimu Katibu huyo Msaidizi alisema sambamba na zoezi hilo ilifanyika tathmini ya hatua zilizochukuliwa katika kutatua



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Mbogwe kilichofanyika katika ofisi za TSC wilayani hapo hivi karibuni.*

kero na malalamiko ya walimu yaliyoibuliwa shuleni katika ziara za Ofisi ya Tume Wilayani hapo kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 ambapo Tume ilibaini changamoto katika ulipaji wa stahiki na haki za walimu kama madai ya mapunjo ya mishahara, likizo, uhamisho, upandishwaji vyeo na taratibu za matibabu.

Aidha, alisema katika ziara hiyo waliweza kuongea na Wanafunzi wapatao 5,586 wa Shule nane za Sekondari juu ya masuala yanayohusu shule salama na uzingatifu wa maadili ya Kitanzania ili kupambana na vitendo viovu vya ukatili na unyanyasaji wa kisaikolojia na kijinsia kama ulawiti na ubakaji katika shule na mazingira ya nyumbani ambako wanaishi kwa muda mchache ukilinganisha na muda wanaotumia shuleni wawapo na Walimu.

Vilevile Mwl. Masaza alisema wanafunzi hao walipata fursa kuwasilisha kero zao kwa uwazi huku wengine wakiwasilisha



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Mbogwe kikiwa kinaendelea.*

# SHULE 57 ZAJENGEWA UWEZO WA UFAFANUZI WA KANUNI ZA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU – AS MASAZA



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Mbogwe.*

kwa maandishi ili TSC na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri waweze kuzitafutia ufumbuzi huku akibainisha sehemu ya kero hizo kuwa ni pamoja na utoaji wa adhabu za viboko visivyozingatia Sheria na Taratibu za adhabu.

Akizungumzia eneo la ajira na maendeleo ya walimu katika Wilaya ya Mbogwe alisema kuwa jumla ya Walimu 59 ikiwa ni Walimu 42 wa Shule za Msingi na 17 wa Sekondari walithibitishwa kazini katika Kikao cha Kamati ya Tume ya Wilaya kilichokaa Aprili 28, 2023 baada ya Walimu hao kufanyiwa tathmini na Wathibiti Ubora wa Shule Wilayani humo.

Alisema kuwa katika eneo la hali ya nidhamu ya walimu wilayani humo, ofisi yake katika kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa mujukumu ya mwaka wa fedha 2022/ 2023 ilipokea jumla ya mashauri sita yakiwemo mashauri matatu yanayohusu utoro kazini, mawili yanayohusiana na ukiukwaji wa taratibu za kuwaondoa shuleni wanafunzi watoro na kushindwa kutoa taarifa kwa mwajiri juu ya utoro wa mwanafunzi na moja kwa kushindwa kuwasilisha kwa mwajiri cheti cha kidato cha nne.

Akihitimisha uwasilishaji wake Mwl. Masaza alijivunia mwitikio na mapokeo chanya ya Walimu wilayani humo katika huduma wanazopatiwa na Ofisi yake akibainisha kuwa wamekuwa na ushirikiano mzuri nawa haraka, wamekuwa wazingatiaji wazuri wa kutekeleza maelekezo yote wanayowapatia, wanatambua na kuthamini kazi inayofanywa na TSC Mbogwe, wanawasilisha kero na malalamiko kwa uwazi na ushiriki wao mkubwa katika masuala ya Kitaifa na Kijamii.

Zoezi la uhamasishaji na utoaji elimu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma ni endelevu. Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu utatumika kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walioajiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara, Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu pamoja na Wadau wa Elimu katika ngazi mbalimbali.



# KATIBU TAWALA KATAVI AISHAURI TSC KUENDELEA KUELIMISHA WALIMU JUU YA VITENDO VYA UKATILI

**Na Mwandishi wetu – Mpanda, Katavi**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi, Hassan Abas Rugwa ameishauri Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuweka msisitizo katika kutoa elimu kwa walimu juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia hususan kwa watoto ili kukomesha vitendo hivyo na kufanya wanafunzi kuwa na mazingira salama wakati wote.

Rugwa ametoa ushauri huo Mei 31, 2023 katika kikao chake na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama aliyefika ofisini kwa Katibu Tawala huyo kutokana na kuwepo kwake mkoani hapo kwa ajili ya kikao kazi cha wadau wa elimu cha kupitia rasimu ya Ufafanuzi wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016 kinachofanyika kwa siku tatu, Mei 31 – Juni 2, 2023 mjini Mpanda.

Rugwa alisema katika jamii ya sasa kumekuwa na matukio mengi ya ukatili ikiwemo ubakaji, ulawiti na vipigo ambapo kwa kiasi kikubwa watoto ndio wamekuwa waathirika.

"Kila siku tunasikia vitendo vya ukatili vinavyotokea hapa nchini. Watu wazima wanawafanyia watoto lakini pia hata watoto kwa watoto wanafanyiana vitendo vya ubakaji na ulawiliti. TSC mna jukumu kubwa la kufanya, kwanza kutoa elimu kwa walimu ili wasijihusishe na vitendo hivyo, pili kuhakikisha walimu wanakuwa mstari wa mbele kuchukua hatua ikiwemo kutoa taarifa kwenye mamlaka husika pale vitendo hivyo vinapotokea na tatu kuwaelimisha watoto kijitambua, kujiepusha na vitendo hivyo pamoja na kutoa taarifa pale mambo hayo yanapotokea," alisema.

Aliongeza kuwa walimu ndio msingi wa kujenga maadili mema kwa jamii kwa kuanzia na watoto, hivyo ni muhimu kuhakikisha juhudi za kupambana na vitendo hivyo zinaanzia kwa walimu.

Alikwenda mbali na kusisitiza kuwa kama ipo haja ya kufanya marekebisho kwenye Sheria au Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu ni vyema kufanya hivyo ili walimu wapewe kipaumbele katika kusaidia jamii kuondokana na tabia hizo za mmomonyoko



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi, Hassan Abas Rugwa akizungumza katika kikao chake na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwaza kushoto) kilichofanyika Mei 31, 2023 katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi zilizopo katika Manispaa ya Mpanda. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Katavi, Mwl. Upendo Rweyemamu.*

# KATIBU TAWALA KATAVI AISHAURI TSC KUENDELEA KUELIMISHA WALIMU JUU YA VITENDO VYA UKATILI



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akifafanua jambo wakati wa kikao kifupi kati yake na Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi (hayupo pichani) kilichofanyika Mei 31, 2023 katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa Katavi iliyopo Manispaa ya Mpanda.*

wa maadili.

"Mnapokwenda kwenye kazi yenu ya ufafanuzi wa Sheria na Kanuni za Tume angalieni namna masuala haya ya elimu dhidi ya ukatili yanavyopata kipaumbele kwa walimu ili kusaidia kuokoa jamii, sote tunajua kwamba masuala haya ni kinyume na utamaduni na maadili yetu ya Kitanzania," alisisitiza.

Akizungumzia hali ya walimu katika Mkoa huo, Rugwa alisema Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kufanya kazi vizuri jambo ambalo limeleta utulivu kwa watumishi hao kutokana na kutatuliwa changamoto zao kwa wakati.

"Katika Mkoa wetu walimu wanaendelea kutekeleza majukumu yao katika hali ya utulivu. Hata mimi nafarijika kuona hali hii ya utulivu na inanifanya nipate muda mwingi wa kufuatilia shughuli zingine za maendeleo ya wananchi. Ingekuwa hali siyo nzuri muda wote ingekuwa ni kukaa ofisini kusikiliza matatizo ya walimu. Simaanishi kwamba walimu hawana changamoto, lakini tumeendelea kuzitatua kwa kiwango ambacho kinawaridhisha," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema watazingatia na kutoa msukumo mkubwa katika kutoa elimu kwa walimu ili kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa watoto na jamii kwa ujumla.

Pia, alimshukuru Katibu Tawala huyo kutokana na ushirikiano wanaoutoa kwa Ofisi za TSC zilizopo katika wilaya za Mkoa wa Mpanda.

Mwl. Nkwama alifika katika ofisi hiyo akiwa ameambatana na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Fatuma Muya, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mpanda, Benson Ng'amilo pamoja na maafisa wengine kutoka TSC Makao Makuu.



*Kikao cha Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi na Katibu wa TSC kikiwa kinaendelea.*

# KATIBU TSC AKUTANA NA WATUMISHI WA TTU WANAOFANYA UTAFITI

**Na mwandishi wetu – Dodoma.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amekutana na kufanya mazungumzo na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Umma (TUU) waliofika katika ofisi za Katibu huyo tarehe 10 Mei, 2023.

Watumishi hao kutoka TUU walifika katika ofisi za Katibu huyo kwa lengo la kusambaza madodoso kwa watumishi wa TSC yanayohusu utafiti unaofanywa na TUU juu ya sababu zinazochangia utoro kwa watumishi wa umma.

Katika mazungumzo hayo, Mwl. Nkwama alieleza kuwa kufanya utafiti ni jambo muhimu kwa maendeleo ya taasisi kwani ndiyo njia sahihi inasaidia kujua changamoto na namna ya kuzitatua.

Watumishi hao walieleza kuwa suala la utoro kwa watumishi wa umma ni kubwa kwani linachukua zaidi ya asilimia 70 ya rufaa wanazopokea na ndiyo sababu iliyoleta msukumo wa kufanya utafiti huo ili kujua sababu zinazosababisha tatizo hilo na kupata njia ya kukabiliana nalo.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Umma (TUU) (wa kwanza kushoto na wa kwanza kulia) wakati watumishi hao walipotembelea TSC hivi karibuni. Wengine ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC (wa pili kutoka kulia), Fatma Muya na Afisa Utumishi wa TSC, George Ndatta (wa pili kutoka kushoto).*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Umma (TUU) (wa mwisho kushoto na wa mwisho kulia) wakati watumishi hao walipotembelea TSC hivi karibuni.*





*Kikao cha Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na watumishi kutoka Tume ya Utumishi wa Umma (TUU) kikiwa kinaendelea.*

# WAKADIRIAJI MAJENZI WADAIWA KUTOTOA TATHMINI SAHIHI ZA MAHITAJI YA UKARABATI WA JENGO LA OFISI YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYANI MANYONI

- *Yadaiwa ni kutokana na kazi hizo kutofanywa chini ya ukandarasi wa halmashauri baada ya tathmini na ukadiriaji huo;*
- *Shule za Msingi 19 kati ya 145 na Shule za Sekondari 17 kati ya 30 zafikiwa;*
- *Jumla ya Walimu 232 kati ya 1,172 (19.8%) wa Msingi na Walimu 224 kati ya 474 (47.3%) wa Sekondari wapatiwa Elimu ya Kanuni;*
- *Lengo ilikuwa kuwafikia Walimu 1,546 kabla ya Mwaka wa Fedha 2022/ 23 kumalizika;*
- *Changamoto kuwafikia Walimu yabainika kuwa ni usafiri na miundombinu duni kutoka eneo moja hadi jingine;*
- *Kati ya Walimu 683 ni Walimu 187 tu ndiyo waliopandishwa cheo huku wawili wakipoteza sifa mchakatoni kwa kupata mashauri;*
- *Kwa kipindi cha miaka mitatu Walimu wanaume wanaongoza kwa mashauri ya nidhamu huku Walimu wa Shule za Sekondari na kosa la utoro vikishika hatamu;*
- *Yaelezwa uhamasishaji na utoaji elimu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma ni endelevu.*

**Na. Mwandishi Wetu – Manyoni.**

Wakadiriaji Majenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Mkoani Singida wamedaiwa kutotoa tathmini sahihi za mahitaji ya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani humo kutokana na kile kinachoaminiwa kazi hizo kutofanywa chini ya ukandarasi wa halmashauri baada ya tathmini na ukadiriaji huo.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilayani Manyoni, Ndg. Hawa Sufiani Rajabu, akizungumza na kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa utoaji elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa ufadhili wa Mradi wa BOOST wilayani humo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, katika ziara zake za kila mwezi kupata habari za utendaji kazi wa Ofisi za Wilaya.

"Tumekua na changamoto ya muda mrefu na Wakadiriaji Majenzi wa Halmashauri ya Wilaya yetu hapa kila tunapowaomba kuja kufanya tathmini 'report' wanazowasilisha zinakua na mashaka makubwa kwani katika hali ya kawaida katika soko gharama zinazowekwa kwa jili ya ukarabati zinakua ndogo sana au kubwa sana na baada ya kufuatilia kwa karibu tukabaini matokeo hayo yanatokana na ukweli kwamba wanaamini kuwa baada ya wao kufanya kazi ya tathmini na ukadiriaji wa mahitaji ya ukarabati kandarasi hiyo itafanywa na wataalamu wengine na sio chini ya Halmashauri." Alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo Ndg. Hawa Rajabu



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Manyoni, Hawa Rajab (kulia) akifafanua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo wakati wa kikao cha watumishi wa TSC Manyoni na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Manyoni. Pembeni yake ni Afisa Maadili na Nidhamu wa TSC Manyoni, Enock Tikae.*

# WAKADIRIAJI MAJENZI WADAIWA KUTOTOA TATHMINI SAHIHI ZA MAHITAJI YA UKARABATI WA JENGO LA OFISI YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYANI MANYONI



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa kwanza kulia) akizungumza na watumishi wa TSC Wilaya ya Manyoni wakati wa kikao chake na watumishi hao kilichofanyika hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya ya hiyo.*



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Manyoni kikiwa kinaendelea.*

Akizungumzia utoaji elimu kwa Walimu kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu alisema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu wilayani humo kupitia ziara za shule kwa shule na mihadhara mbalimbali ya Walimu wilayani humo; TSC imefanikiwa kuzifika Shule za Msingi 19 kati ya 145 na Shule za Sekondari 17 kati ya 30 ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na Halmashauri ya Mji wa Itigi zinazohudumiwa na Ofisi hiyo ya TSC huku ikiwafikia Walimu 232 kati ya 1,172 sawa na asilimia 19.8 ya Walimu wa Shule za Msingi na Walimu 224 kati ya 474 sawa na asilimia 47.3 ya Walimu wa Shule za Sekondari ndani ya Halmashauri hizo.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo Ndg. Rajabu alisema kuwa malengo ya TSC Wilayani humo yalikuwa ni kuwafikia Walimu 1,546 na kuwapatia elimu hiyo ya ufafanuzi wa Kanuni na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kabla ya Mwaka wa Fedha 2022/ 23 kumalizika huku mpaka sasa wakiwa wamefikiwa Walimu 456 tu ambao ni sawa na asilimia 29.5 ya lengo zima.

# WAKADIRIAJI MAJENZI WADAIWA KUTOTOA TATHMINI SAHIHI ZA MAHITAJI YA UKARABATI WA JENGO LA OFISI YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYANI MANYONI

Alisema, "Changamoto kubwa tuliyonayo kwasasa katika kuwafikia Walimu na kuwapa elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni ni namna ya kuwafikia Walimu hao katika eneo lote la Halmashauri hizi mbili tunazozihudumia kwani usafiri na miundombinu yake kutoka eneo moja hadi jingine ni mgumu sana pamoja na Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya kutoa ushirikiano wa mara kwa mara wa gari kwenda kuhudumia Walimu katika maeneo yao ya kazi kwa kushirikiana na wenzetu wa Udhibiti Ubora, Idara ya Elimu msingi na Sekondari na wakati mwingine Chama Cha Walimu (CWT)."

Vilevile, Ndg. Rajabu alisema kwa Walimu wa Halmashauri mbili zinazohudumiwa na Ofisi yake Wilayani Manyoni yaani Halmashauri ya Wilaya Manyoni na Halmashauri ya Mji Itigi; kati ya Walimu 683 wenye sifa za kupandishwa cheo, jumla wa Walimu 187 tu ndiyo waliopandishwa kutokana na idadi ya 189 iliyowasilishwa (eligibility list) kutoka Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora huku wawili wakipoteza sifa wakati wa mchakato kwa kupata mashauri ya kinidhamu.

Akizungumzia eneo la hali ya nidhamu ya Walimu wilayani humo, alisema kwa mujibu wa takwimu za mashauri ya Walimu katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha kiutekelezaji (2020/21 – 2022/23) ndani ya Wilaya ya Manyoni yenye Halmashauri mbili, Tarafa tano, Kata 19, Vijiji 54, Vitongoji 279, Shule 74 za Msingi na 19 za Sekondari; Ofisi yake imebaini Walimu wanaume kuongoza kwa mashauri ya kimaadili kwa kipindi hicho chote huku Walimu wa Shule za Sekondari wakiongozi kwa idadi ya mashauri na kosa la utoro likishika hatamu likifuatiwa na makosa mengine yakiwemo; kukaidi au kukataa uhamisho, kughushi nyaraka na makosa mengine ya kimaadili.

Zoezi la uhamasishaji na utoaji elimu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma ni endelevu. Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu utatumika kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walioajiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara, Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu pamoja na Wadau wa Elimu katika ngazi mbalimbali.




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Manyoni.*

# TSC YAANDAA NYARAKA ZA KUSIMAMIA MAENDELEO YA TEHAMA

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ipo katika hatua za mwisho za kuandaa nyaraka mbalimbali zinazohusu usimamizi wa maendeleo ya Teknolojia ha Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi hiyo inayosimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali.

Nyaraka zinazoandaliwa ni Mpango Mkakati wa TEHAMA (ICT Strategic Plan), Sera ya TEHAMA (ICT Policy) pamoja na Sera ya Ulinzi wa TEHAMA (ICT Security Policy).

Kazi hiyo inafanywa na timu ya wataalamu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) pamoja TSC.

Akizungumza wakati wa utekelezaji wa kazi hiyo, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema kukamilika kwa nyaraka hizo kunaisaidia Tume kuendana na Malengo ya Serikali ya kuongeza matumizi ya TEHAMA



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akifafanua jambo wakati wa Kikao kazi cha kuandaa nyaraka za TEHAMA za Tume. Kikao Kazi hicho kimefanyika mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.*



*Mratibu wa Kikao Kazi cha kuandaa nyaraka za TEHAMA za TSC ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA cha Tume hiyo, Kainda Ndasa (wa kwanza kulia) akiwa katika kikao kazi hicho kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.*

# TSC YAANDAA NYARAKA ZA KUSIMAMIA MAENDELEO YA TEHAMA

katika shughuli za Serikali.

Aliongeza kuwa nyaraka hizo zitasaidia kuonesha mikakati ya kuweka miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za TSC Makao Makuu na wilayani na hivyo kuongeza matumizi ya teknolojia hiyo ambayo inaondoa gharama za kutumia karatasi na kusaidia kutoa huduma kwa muda mfupi.

Pia alisema nyaraka hizo zitasaidia watumishi kuelewa namna bora ya kutunza vifaa vya TEHAMA ili vidumu kwa muda mrefu pamoja na kuelewa matumizi sahihi ya mtanado wa intaneti wa ofisi kwa mujibu wa sheria na taratibu.

"Nyaraka hizi ni muhimu sana kwetu katika kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa walimu. Tunatamani tufike sehemu mwalimu aweze kupata huduma zetu pale pale alipo kwa kutumia simu yake ya mkononi. Hii itasaidia walimu wetu waendelee kutulia kwenye vituo vya kazi badala ya kutumia muda wa kufundisha kwenda ofisi mbalimbali kwa ajili ya kutatuliwa changamoto zao," alisema Nkwama.



*Kikao Kazi cha kuandaa nyaraka za TEHAMA za TSC kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kikiwa kinaendelea*



*Kikao Kazi cha kuandaa nyaraka za TEHAMA za TSC kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kikiwa kinaendelea.*

# SENYAMULE AAGIZA UJENZI WA MADARASA KUKAMILIKA KWA WAKATI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, ameendelea na ziara zake za kikazi za kukagua maendeleo ya ujenzi wa mabweni katika Shule ya Wasichana Bunge, ujenzi wa Shule mpya ya msingi katika eneo la Swaswa na madarasa ya awali katika Shule ya Msingi Kisasa ambapo ujenzi wake uko katika hatua za ukamilishaji.

Katika kaguzi hizo Mhe. Senyamule alitoa maagizo kwa wasimamizi wa mradi kuhakikisha kazi inakamilika kwa muda uliopangwa na kuzingatia viwango vya ubora huku akitoa rai kwa wasimamizi wa ujenzi kukaa na mafundi ili kufanikisha ukamilishaji wake.

"Mkoa wa Dodoma tumejipanga kukamilisha hizi kazi kwa wakati hivyo wataalamu mkae na mafundi mpitie kwa pamoja mpango kazi wa miradi hii ili tujue kila siku ni kazi gani inatakiwa kukamilika kwa siku husika ili itakapofika tarehe 15 Juni 2023 ujenzi uwe umekamilika" Senyamule amesisitiza.

Aidha, Senyamule amesema kuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa fedha zote kwa wakati hivyo hakuna sababu za kuchelewa kufanya manunuzi. Amesema ni wajibu wa wataalamu kuhakikisha ununuzi wa vifaa vyote vinavyohitajika vinapatikana ili mradi uweze kukamilika kwa muda uliopangwa.

Mkoa wa Dodoma kupitia mradi wa Boost umepokea kiasi cha Shilingi Bilioni 10.6 kwa ajili ujenzi wa Shule mpya 16, vyumba vya madasa ya msingi 163, madarasa ya awali 16, ujenzi wa vyoo 106, nyumba za walimu 03 na darasa 01 la elimu maalumu.

Shule ya Msingi Kisasa imepokea kiasi cha Shilingi Milioni 63.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 na vyoo 6 huku Shule ya Swaswa imepokea kiasi cha Shilingi Milioni 318.8 kwa ajili ya kujenga Shule mpya itakayokuwa na madarasa ya msingi 7, madarasa ya awali 2 na Vyoo 12.















# TSC BUHIGWE YAFANYA ZIARA SHULE YA SEKONDARI MHARULO

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Buhigwe tarehe 12 Mei, 2023 ilifanya ziara katika Shule ya Sekondari Mharulo iliyopo Kata ya Mkatanga na kuongea na wanafunzi juu ya masuala mbalimbali ya maendeleo ya kitaaluma na maadili kwa wanafunzi hao.








*Wanafunzi wa Mharulo wakipata elimu kutoka kwa Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Buhigwe.*

# MENEJIMENTI YA TSC YAPATIWA MAFUNZO YA e – BOARD

Wajumbe wa menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamepatiwa mafunzo ya e – board yaliyolenga kuongeza matumizi ya teknolojia katika utendaji kazi wa majukumu ya Tume.

Mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 15 Mei, 2023 yanatarajiwa kuisaida Tume kupunguza gharama za uendeshaji kutokana kuondokana na matumizi ya karatasi.









*Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakipata mafunzo ya e – Board yaliyofanyika tarehe 15 Mei, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC Makao Makuu.*

# IFAHAMU TSC IKUNGI NA JUHUDI ZA KUELIMISHA, KUSIMAMIA MASLAHI YA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Ikungi.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ikungi ni miongoni mwa Ofisi za Tume zinazopatikana ndani ya Mkoa wa Singida. Ofisi hiyo inahudumia jumla ya walimu 1,524 ambapo kati ya hao, walimu 962 ni wa shule za msingi na walimu 562 ni wa shule za Sekondari. Walimu hao wanafundisha wanafunzi katika shule za msingi 125 na shule za sekondari 32 za Serikali.

Itakumbukwa kuwa tarehe 24 Januari, 2023 Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kilichoandaliwa na TSC kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa BOOST kilizinduliwa. Kitabu hicho kina lengo la kuwasaidia walimu kuelewa kwa kina na kuzingatia maadili ya utumishi wao.

Uzinduzi huo uliambatana na kikao kazi cha siku nne cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka Wilaya zote Tanzania Bara ambao walipatiwa mafunzo juu ya Ufafanuzi huo ili nao wakawaelimishe walimu katika maeneo yao ya kazi.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kushoto) akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ikungi, Stella Mollel wakati wa kikao cha watumishi wa TSC wa Wilaya hiyo na Mkuu huyo wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kilicholenga kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya ya Ikungi.*

Stella Mollel ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ikungi ambaye alihudhuria mafunzo hayo na mara baada ya kumaliza mafunzo alianza utekelezaji wa kutoa elimu kwa walimu katika shule mbalimbali za msingi na sekondari ndani ya Wilaya hiyo.

Akizungumza wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami ambaye alifika ofisini hapo kwa lengo kupata taarifa ya namna



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ikungi, Stella Mollel (katikati) akifafanua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo wakati wa kikao cha watumishi wa TSC Ikungi na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kushoto) kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Ikungi.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ikungi, Stella Mollel (kulia) akifafanua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo wakati wa kikao cha watumishi wa TSC Ikungi Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kushoto) kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Ikungi.*

# IFAHAMU TSC IKUNGI NA JUHUDI ZA KUELIMISHA, KUSIMAMIA MASLAHI YA WALIMU

zoezi la utoaji elimu kwa walimu linavyofanyika, Stella alieleza kuwa katika kipindi hicho kifupi ofisi yake imezifikia shule 73 kati ya 125 za msingi na 21 kati ya 32 za sekondari.

"Jumla ya walimu 589 kati ya 962 wa shule za msingi na 347 kati ya 561 wa shule za sekondari tumewapatia elimu hiyo. Shule ambazo hatujazifikia ni 52 za msingi na 11 za sekondari ambazo tumepanga kuzifikia katika kipindi cha mwezi mmoja kuandia tarehe 24 Julai hadi tarehe 24 Agosti, 2023," alisema.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alifafanua kuwa sababu kubwa ya kufanikiwa kuwafikia walimu wengi kwa muda mfupi ni ushirikiano uliopo kati ya ofisi yake na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ambapo amekuwa akiambatana na maafisa elimu katika kufanya ziara shuleni.

Alisema pamoja na mfanikio ya kuwafikia walimu, ofisi yake imeendelea kusimamia stahiki za walimu kama malipo ya likizo ambapo kwa sasa walimu wanalipwa kabla ya kuanza likizo, pia ofisi yake imekuwa ikishirikishwa kikamilifu katika mchakato wa uteuzi wa walimu wakuu na wakuu wa shule jambo ambalo limesaidia kupatikana kwa viongozi wa shule wenye uwezo wa kusimamia maadili ya walimu.

Pamoja na mafanikio hayo, Stellah alieleza kuwa ipo changamoto kwa baadhi ya walimu wachache ambao bado wanajihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa madili ya kazi ya ualimu, kwa mfano mwaka 2020/2021 kulikuwa na mashauri ya nidhamu manne (4), mwaka 2021/2022 hapakuwa na shauri lakini mwaka huu 2022/2023 ambao bado haujamalizika tayari kuna mashauri sita (6).

"Ukiangalia mashauri haya, kosa linaloongoza ni utoro kazini. Wapo walimu wanaoacha kazi bila kuzingatia utaratibu baada ya kupata kazi nyingine lakini tumegundua wapo walimu wanaojiingiza kwenye utoro kutokana na kuwa na madeni yanayosababishwa na kukopa bila kuzingatia sheria na taratibu. Wanaposhindwa kulipa madeni wanaamua kutoroka ili kuwakwepa wale wanaowadai," alisema Stella.

Aliendelea kufafanua kuwa, katika ziara za utoaji elimu juu ya ufafanuzi wa Kanuni za maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu, msisitizo umewekwa katika kuwaelimsha walimu juu ya taratibu za kukopa na kuwasihi waachane na tabia ya kukopa katika taasisi zisizorasmi.

Akielezea kuhusu ajira na maendeleo ya walimu Stella aliishukuru Serikali kwa namna inavyojitahidi kutatua chngamoto ya upungufu wa walimu na kujali maslahi ya yao katika Wilaya ya Ikungi ambapo mwezi Julai 2022 walimu 144 waliajiriwa na katika idadi hiyo walimu 118 walikuwa wa shule za msingi na 26 wa sekondari.

"Katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 tumepandisha vyeo walimu 384 ambapo katika idadi hiyo, walimu 311 ni wa shule za msingi na 73 ni wa sekondari. Walimu 317 wameidhinishwa katika mishahara ya vyeo vyao vipya mwezi Mei, 2023. Taratibu za kuwaidhinishia mishahara ya vyeo vipya kwa walimu 67 waliobaki zinaendelea kufanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora," alisema.



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Ikungi kikiwa kinaendelea.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Ikungi.*

# TSC NAMTUMBO YATOA ELIMU KWA WANAFUNZI WA SHUE YA SEKONDARI SELOUS

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Namtumbo imefanya ziara katika shule ya Sekondari Selous ambapo pamoja na mambo mengine imetoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Selous kuhusu namna maadili mema yanavyochangia katika maendeleo ya taaluma kwa mwanafunzi mmoja mmoja na shule kwa ujumla.




*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Namtumbo, Abel Nyoni akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Selous kuhusu namna maadili yanavyochangia katika maendeleo ya taaluma ya wanafunzi.*




*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Selous wakimsikiliza Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Namtumbo, Abel Nyoni (hayupo pichani) ambapo kiongozi huyo alizungumzia umuhimu wa maadili katika maendeleo ya taaluma mwanafunzi.*

# TSC CHAMWINO YAENDELEA KUTOA ELIMU KWA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Chamwino imeendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utedaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma.

Tarehe 15 na 16 Mei, 2023 ofisi hiyo ilifanya ziara katika tarafa mbili (02), kata 16 na shule 73 ambapo jumla ya walimu 877 wa shule za Msingi na Sekondari walipatiwa mafunzo.

Wadau wengine walioshiriki ziara hiyo ni Afisa Elimu wa Mkoa, Maafisa Elimu wilaya, Wathibiti Ubora wa Shule huku Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI anayehusika na Elimu, Dkt. Charles Msonde akishiriki kwa njia ya simu ambapo aliwapongeza walimu kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuwahudumia wanafunzi huku akiwasisitiza kuzingatia Miongozo, Sheria, Taratibu na Kanuni wakati wa kutimiza majukumu yao.

Taarifa ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Chamwino, Paulina Kanumba kuhusu utekelezaji wa kazi hiyo ilieleza kuwa lengo kuu la utoaji wa elimu hiyo ni kuhakikisha walimu wote 1800 wa Wilaya ya hiyo wanakuwa na mwenendo na tabia njema katika utumishi wa umma.

"Baada ya mafunzo kila mwalimu anatakiwa aweze: Kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma; Kutimiza majukumu yake ya ufanisi, uzalendo, uadilifu na kutenda haki kwa kuzingatia sheria na kanuni; Kuwajibika ipasavyo kwa taaluma yake, kwa watumishi wenzake, kwa mwajiri, kwa wazazi na walezi wa wanafunzi, kwa jamii inayomzunguka, kwa Taifa na kwa Mkuu wa Shule au mwalimu mkuu; na Kuzingatia kanuni za maadili na utendaji kazi wa walimu bila kuzikiuka," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Mafunzo hayo yalitumia zana mbalimbali za kufundishia ikiwemo picha, projekta, vitabu vya kanuni na sheria pamoja na vipeperushi huku njia za ufudishaji zikiwa ni majadiliano, mihadhara na maswali na majibu.

# WIZARA YA ELIMU YATOA MAFUNZO KWA WALIMU 500 MATUMIZI YA VISHKWAMBI

- *Agizo la Rais Samia latekelezwa*

**Na. Mwandishi Wetu – Arusha.**

Walimu zaidi ya 500 wa shule za sekondari nchini wameanza kupatiwa mafunzo ya matumizi sahihi ya Tehama na Vishkwambi ili kupata mbinu mpya za kufundishia.

Mafunzo hayo yamekuja ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa siku ya Mei Mosi 2023 baada ya kusoma moja ya bango la walimu walioomba kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kutumia vishkwambi kufundishia.

Akifungua mafunzo hayo mkoani Arusha, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Rwezimula amesema mafunzo hayo ya siku tano yanalenga kuwafundisha walimu 1500 walioko kazini mbinu mpya za matumizi ya TEHAMA na vishkwambi katika kufundishia na kujifunza ili nao wakafundishe wenzao.

"Mafunzo haya yako chini ya Mradi wa miaka mitano unaolenga 'kuboresha mazingira ya ujifunzaji, ufundishaji kwenye shule zetu za sekondari' (SEQUIP), ikiwa ni utekelezaji wa mapinduzi makubwa ya Elimu".

Dkt. Rwezimula aliwataka walimu hao kuwa makini katika mafunzo ili yakalete tija na wakawe mabalozi wazuri kwenye maeneo yao ya kazi.

"Dunia imezama kwenye Sayansi na Teknolojia, hivyo wizara inategemea kuwanoa ninyi ili muenende na mabadiliko hayo, hivyo basi na nyie bebeni dhamana ya kwenda kuwasaidia wenzenu".

Kwa upande wake Mratibu wa SEQUIP, Dkt Mollel Meigaru alisema kuwa Mafunzo hayo yanayolenga kuimarisha Elimu ya sekondari nchini chini ya ufadhili wa benki ya dunia kwa mkopo wa dola milioni 500.

"Mbali na mafunzo haya, pia mradi umefanikisha kutoa mafunzo kwa walimu 18,000 juu ya namna bora ya kufundisha masomo ya sayansi, na kuhusisha na TEHAMA, lakini pia unalenga kujenga miundo mbinu kwa shule za sekondari ambapo unajenga shule 1000 za mchanganyiko na zingine 26 za wasichana kila mkoa" alisema.

Alisema mafunzo hayo kwa walimu yanatarajia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi hasa wa masomo ya Sayansi na kwenda kuwa msaada mkubwa kwa Taifa baadae.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Elimu maalum Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Magreth Matonya aliwataka walimu wenye mahitaji maalum waliopata nafasi ya kuhudhuria mafunzo hayo wakawe wakufunzi wazuri.

# WATAFITI KUTOKA DATA VISION INTERNATIONAL WAMTEMBELEA KATIBU TSC

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amekutana na kufanya mazungumzo na wataalamu wa masuala ya Utafiti kutoka Taasisi isiyo ya Serikali, Data Vision International waliofika ofisi za TSC tarehe 09 Mei, 2023.

Watafiti hao walifika Ofisi za TSC Makao Makuu ikiwa ni sehemu ya utafiti wao unaohusu masuala ya elimu. Katika Kikao hicho Katibu wa TSC aliwapatia maelezo na nyaraka mbalimbali zinazohusu utumishi wa walimu ili kuwasaidia kukamilisha utafiti wao.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye miwani) akizungumza na wataalamu wa masuala ya Utafiti kutoka taasisi isiyo ya Serikali, Data Vision International waliofika ofisi za TSC tarehe 09 Mei, 2023.*







*Kikao cha Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama na wataalamu wa masuala ya Utafiti kutoka taasisi isiyo ya Serikali, Data Vision International waliofika ofisi za TSC tarehe 09 Mei, 2023 kikiwa kinaendelea.*

# MILIONI 940 KUBORESHA ELIMU YA AWALI NA MSINGI SERENGETI



**Na. Mwandishi Wetu – Serengeti.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, amesema Serikali kupitia Mradi wa Kuimarisha Ujifunzaji katika Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) imepeleka shilingi milioni 940.9 katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara kwa ajili ya kuboresha Elimu ya Awali na Msingi.

Aliyasema hayo hivi karibuni wakati akiongea na Wananchi wa Kijiji cha Bisarara Wilayani Serengeti wakati alipoambata na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ili kusikiliza na kutatua kero za Wananchi Mkoani Mara.

"Mradi huu wa BOOST unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, utagharimu kiasi cha shilingi trilioni 1.15 ambapo katika kipindi hiki cha mwezi Mei tayari Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imeletewa shilingi milioni 940.9 kuboresha Elimu ya Awali na Msingi." Alisema Waziri Kairuki.

Kairuki alisema katika fedha hizo za Mradi wa BOOST, shilingi milioni 540.3 zitatumika kujenga Shule ya Msingi Mapinduzi B yenye mikondo miwili katika Kata ya Mugumu, milioni 300 zitajenga Vyumba vya Madarasa 12 katika Shule za Kambarage, Kisaka, Mapinduzi, Monunu na Remung'oroti na shilingi milioni 69.1 zitajenga Madarasa mawili ya Awali katika Shule ya Remung'oroti huku akifafanua kuwa shilingi milioni 31.5 zitatumika kujenga matundu ya vyoo 15.

Aidha, Waziri Kairuki alisema shilingi milioni 470 kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ilipelekwa katika Wilaya Serengeti ili kujenga Shule Mpya ya Sekondari ya Morotonga ambayo Wanafunzi zaidi ya 80 wameshaanza masomo katika shule hiyo.

Waziri Kairuki alisema, shilingi milioni 600 zitapelekwa katika Kata ya Nagusi ili kujenga Shule Mpya ya Kata ambazo alisema zitapelekwa katika awamu mbili, ambapo Awamu ya Kwanza itapelekwa shilingi milioni 470 na Awamu ya Pili itapelekwa milioni 130 ambayo itajenga Nyumba ya Walimu na kununua Vifaa vya TEHAMA.











# TSC GEITA YATOA ELIMU KWA WALIMU SHULE ZA MWALONI, IHUMILO NA LUHULA



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Geita, Sitta Musanga akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya ya Geita wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) iliyofanyika wilayani hapo hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji ya majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Geita kilichofanyika katika ofisi za TSC wilayani hapo hivi karibuni.*

**Na Mwandishi wetu – Geita.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Geita imefanya ziara katika shule za Mwaloni, Ihumilo na Luhula zilizopo katika Halmashauri ya Mji wa Geita kwa lengo la kutoa elimu kuhusu Ufanafuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.

Vile vile Ofisi hiyo imefanikiwa kutoa elimu hiyo kwa walimu 19 wa Ajira mpya walioajiriwa mwezi Julai, 2022, Wakuu wa Shule kutoka Halmashauri ya Mji na Wilaya pamoja na Maafisa Elimu Kata kwa lengo la kusaidia walimu kuelewa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Hayo yamebainishwa katika taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya ya Geita iliyowasilishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume Wilaya ya Geita, Sitta Mussanga wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami iliyofanyika tarehe 19, Mei, 2023.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa utoaji elimu umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya TSC wilayani hapo na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Geita ambacho kimewezesha ziara hizo kwa kutoa usafiri.

"Mipango yetu kwa sasa ni kuzifikia kata tano ambazo bado hatujazifikia katika kutoa elimu juu ya Ufanafuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Geita kikiwa kinaendelea.*

# TSC GEITA YATOA ELIMU KWA WALIMU SHULE ZA MWALONI, IHUMILO NA LUHULA



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Geita kikiwa kinaendelea.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Geita, Sitta Musanga akizungumza wakati wa kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami na Watumishi wa Tume Wilaya ya Geita kilichofanyika hivi karibuni.*

Utumishi wa Walimu. Kata hizo ni Nyamalimbe, Bujula, Butobela, Bukoli na Nyarugusu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa upande wa Nidhamu taarifa hiyo ilionesha uwepo wa mshauri ya nidhadhu ya walimu ambapo kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Aprili, 2023 jumla ya mashauri 21 yalifunguliwa huku kosa la utoro likiongoza.

Kuhusu masula ya Ajira Maendeleo, walimu 159 waliajiriwa mwezi julai, 2023 ambapo katika idadi hiyo walimu 119 waliajiriwa Halmashauri ya Mji Geita na walimu 40 waliajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Walimu hao walisajiliwa na tayari wamethibitishwa kazini.

"Kikao cha Kamati ya Wilaya kilichofanyika tarehe 28 Aprili, 2023 kiliwapandisha vyeo walimu 1,041 ambao ndiyo idadi iliyowasilishwa kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Idadi hiyo ni kati ya walimu 1684 waliokuwa na sifa za kupanda. Walimu waliobaki tunaendelea kufanya mawasiliano na mamlaka zingine ili nao waweze kupandishwa kwa kuwa wana sifa tayari," ilisema taarifa hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Geita inahudumia Halmashauri mbili (02) ambazo ni Halmashauri ya Mji Geita na Halmashauri ya Wilaya Geita. Halmashauri zote mbili zina jumla ya walimu 2,857 wanaofundisha shule za msingi 293 huku walimu wa shule za Sekondari wakiwa ni 1,225 kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi katika shule 95.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Geita.*

# TSC NAMTUMBO YAWAFIKIA WALIMU LUEGU, LITOLA NA NAMABENGO

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Namtumbo tarehe 16 Mei, 2023 ilifanya ziara katika kata za Luegu, Litola na Namabengo kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu wa maeneo hayo kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Namtumbo wakitoa elimu kwa walimu wakati wa mafunzo yaliyofanyika tarehe 16 Mei, 2023 katika Shule ya Msingi Luegu.*









*Walimu kutoka kata za Luegu, Litola na Namabengo wakipatiwa mafunzo na watumishi wa TSC (hawapo pichani) tarehe 16 Mei, 2023 katika Shule ya Msingi Luegu.*

# TSC NYANG'HWALE YATOA ELIMU KWA WALIMU 313 NDANI YA MIEZI MIWILI

- *Maafisa Elimu Kata 15*
- *Wakuu wa Shule za Msingi 21*
- *Wakuu wa Shule za Sekondari 4*
- *Walimu wa kawaida Shule za Msingi 185*
- *Walimu wa kawaida Shule za Sekondari 88*

**Na Mwandishi wetu – Nyang'wale.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nyang'wale imefanikiwa kuwajengea uwezo walimu 313 wa shule za Msingi na Sekondari kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu katika mwezi Aprili na Mei, 2023.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyang'wale, Shija Ngassa wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami iliyofanyika katika ofisi hiyo hivi karibuni.


Alisema idadi hiyo inahusisha Maafisa Elimu Kata (15), Wakuu wa Shule za Msingi (21), Wakuu wa Shule za Sekondari (4), Walimu wa kawaida Shule za Msingi (185) pamoja na Walimu wa kawaida Shule za Sekondari (88).

"Miongoni mwa mada tulizowasilisha wakati wa kutoa elimu ni ukiukwaji wa maadili na hatua za kinidhamu; Shule salama na wajibu wa mwalimu ikwa mwanafunzi; Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma; Muundo wa Tume ya Utumishi wa walimu; na Nyaraka muhimu za kiutumishi anazopaswa kuwa nazo mwalimu," alisema Ngassa.

Ngassa aliendelea kusema kuwa elimu hiyo imesaidia kuongeza uelewa kwa walimu kitu kinachofanya waweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa walimu na kujiepusha na ukiukwaji wa maadili ya ualimu.

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Msaidizi huyo, hali ya nidhamu kwa walimu wa wilaya hiyo ni nzuri kutokana na kuwepo kwa idadi ndogo ya mashauri ya nidhamu yaliyofunguliwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2022/2023. Anaamini kwamba kadri wanavyoendelea kutoa elimu hiyo, mashauri yatazidi kupungua.

"Hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya ya Nyang'hwale kwa



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nyang'hwale, Shija Ngassa akizungumzia utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya Nyang'hwale wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) iliyofanyika wilayani hapo hivi karibuni.*

# TSC NYANG'HWALE YATOA ELIMU KWA WALIMU 313 NDANI YA MIEZI MIWILI



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Nyang'hwale kilichofanyika katika ofisi za TSC wilayani hapo hivi karibuni.*



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Nyang'hwale kikiwa kinaendelea.*

ujumla ni nzuri na inaridhisha. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2022/2023 ni mashauri saba (7) tu ndiyo yaliyofunguliwa na matano (5) kati ya hayo yalihitimishwa. Mashauri manne (4) yalikuwa mwaka 2020/2021 na mashauri matatu (3) yamefunguliwa katika mwaka huu 2022/2023," alisema.

Pamoja na hayo, kiongozi huyo aliongeza kuwa mkakati mkubwa unaoendelea sasa ni kutoa elimu kwa Wakuu wa Shule juu ya namna ya kushughulikia mashuri ya nidhamu katika ngazi ya shule kama inavyoelekezwa na Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na kanuni zake za mwaka 2016.

"Katika kuimarisha tabia njema na mwenendo bora wa mwalimu, kila mkuu wa shule amepatiwa nyaraka mbalimbali za kumsaidia kutimiza wajibu wao kama mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu," alisema.

Wilaya ya Nyang'hwale ina jumla ya walimu 1,046 wanaofundisha shule za msingi na sekondari za Serikali. Kati ya hao, walimu 793 ni wa shule za msingi na 253 wa shule za sekondari. Idadi ya shule za msingi za serikali zilizopo kwenye wilaya hiyo ni 74 na sekondari ni 15 huku idadi ya wanafunzi wa shule za msingi za Serikali ikiwa ni 54,870 na sekondari ni 8,906.



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Nyang'hwale kikiwa kinaendelea.*

# KATA 17 ZENYE SHULE 117 WILAYANI BUKOMBE ZAKABIDHIWA VITINI VYA UFAFANUZI WA KANUNI ZA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bukombe, Sungura Matatizo Sungura akizungumza wakati wa kikao cha watumishi wa TSC wa wilaya hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Bukombe.*

**Na. Mwandishi Wetu – Bukombe.**

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Bukombe imefanikiwa kudurufu vitini vya Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu na kuviwasilisha katika Kata zote 17 na Shule zote 117 Wilayani humo ikiwa ni Shule 92 za Msingi na 25 za Sekondari kwa lengo la kuwajengea uwezo wasimamizi wote wa elimu katika Kanuni mpya za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu za mwaka 2023.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilayani Bukombe, Mwl. Matatizo Sungura, alipokuwa akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa utoaji elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa ufadhili wa Mradi wa BOOST wilayani humo alipotembelewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, katika ziara zake za kila mwezi kupata habari za utendaji kazi wa Ofisi za Wilaya.

"Pamoja na ziara tunazofanya shuleni kuwahudumia Walimu katika maeneo yao ya kazi, tumefanikiwa kudurufu vitini vya Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu na kuwakabidhi wadau wote wa Elimu katika Kata zote 17 na Shule zote 117 Wilayani hapa tunazozihudumia ambapo Shule



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kushoto) na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bukombe, Matatizo Sungura wakati wa kikao kilichowakutanisha watumishi wa TSC Wilaya ya Bukombe kilicholenga kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.*

# KATA 17 ZENYE SHULE 117 WILAYANI BUKOMBE ZAKABIDHIWA VITINI VYA UFAFANUZI WA KANUNI ZA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

za Msingi ni 92 naza Sekondari 25 kwa lengo la kuwajengea uwezo wasimamizi wote wa elimu katika Kanuni Mpya za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu za Mwaka, 2023." Alisema Kaimu Katibu Msaidizi Mwl. Sungura.

Mwl. Sungura alisema ufafanuzi huo umetokana na ukweli kuwa Walimu wanapaswa kukumbushwa na kujengewa uwezo zaidi juu ya Kanuni na Sheria zinazohusiana na utendaji kazi wao wa kila siku ili kuepukana na makosa yanayoepukika na hivyo kupunguza au kuondoa mashauri mbalimbali ya kinidhamu na kimaadili yanayosababishwa na Walimu kutokana na kutojua au kutozingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma.

Aliongeza kuwa katika kutekeleza jukumu hilo la uhamasishaji na utoaji elimu kwa Walimu na Wanafunzi, ziara mbalimbali zimekua zikifanyika ikiwa ni sehemu ya juhudi hizo kwa kushirikiana na Maafisa Elimu



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Bukombe kikiwa kinaendelea.*

Msingi na Sekondari ngazi ya Wilaya kwa kuwakusanya Walimu katika Kata tofauti wilayani humo ambapo jumla ya ziara saba zimefanyika kuzifikia kata zote 17.

Mwl. Sungura alisema pamoja na kulifikia kundi hilo pia Ofisi yake kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe iliitisha Kikao Kazi cha uhamasishaji



*Kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu na watumishi wa Tume Wilaya ya Bukombe kikiwa kinaendelea.*

na uelimishaji wa Ufafanuzi wa Kanuni hizo kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata wote ambapo malengo ya mbeleni ni kuendelea kuwafikia Walimu na kuwaelimisha kwa kutembelea Kata mbili kila mwezi.

Kaimu Katibu huyo Msaidizi alisema katika nyanja ya ajira na maendeleo ya walimu katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 mpaka Mei, 2023 jumla ya Walimu 98 (Wanaume 58 na Wanawake 40) waliajiriwa wilayani humo ambapo kati yao Walimu 73 (Wanaume 45 na Wanawake 28) ni Walimu wa Shule za Msingi na Walimu 25 (Wanaume 13 na Wanawake 12) ni Walimu wa Shule za Sekondari.

Vilevile, Mwl. Sungura alisema, "Kwa kipindi hicho cha kuanzia Julai, 2022 hadi sasa Mei, 2023; jumla ya Walimu 503 walipendekezwa kupandishwa vyeo ikiwa ni Walimu Wanaume 295 na Wanawake 208 ambapo kati ya hao 503; Walimu 435

# KATA 17 ZENYE SHULE 117 WILAYANI BUKOMBE ZAKABIDHIWA VITINI VYA UFAFANUZI WA KANUNI ZA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

(Wanaume 248 na Wanawake 187) ni Walimu wa Shule za Msingi na Walimu 68 (Wanaume 47 na Wanawake 21) ni Walimu wa Shule za Sekondari."

Akizungumzia Walimu waliopendekezwa kubadilishiwa vyeo Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa jumla ya Walimu 88 walipendekezwa Wilayani humo ambapo kati yao Walimu 81 (Wanaume 61 na 20 Wanawake) walikuwa ni Walimu wa Shule za Msingi na Walimu saba (Wanaume sita na Mwanamke mmoja) walikuwa ni Walimu wa Shule za Sekondari.

Aidha, taarifa hiyo ilitanabaisha hali ya nidhamu ya walimu wilayani humo kuwa nzuri ukilinganisha na miaka miwili ya nyuma (2020/ 2021 na 2021/ 2022) ambapo takwimu za mashauri kwa miaka hiyo zilikua mashauri 18 kwa matano (5) ukilinganishwa na takwimu za sasa tangu kuanza kwa Utekelezaji wa Mwaka wa Fedha 2022/ 2023 ambapo hadi sasa ni mashauri mawili tu yanayohusiana na utoro ndiyo yaliyopokelewa yakiwahusisha Walimu wawili wanaume mmoja wa shule ya msingi na mwingine sekondari, hii ikibainisha kushuka kwa mashauri ya Walimu kila mwaka wilayani humo.

Mwl. Sungura alijivunia Walimu wa Bukombe kwa kudumisha nidhamu na uadilifu katika utumishi wao, kujituma katika utekelezaji wa majukumu yao, hamasa kubwa waliyonayo katika kujiendeleza kitaaluma na kupenda maendeleo ya jumla.

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ina jumla ya Walimu 1,676 ambapo Walimu 1,113 ni Walimu wa Shule za Msingi (Wanaume 674 na Wanawake 439) huku Shule za Sekondari zikiwa na jumla ya Walimu 563 ambapo Walimu 410 ni Wanaume na 153 ni Wanawake.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Bukombe.*




**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania